**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**(FASIHI)**
**MUDA: SAA: 2½**

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA MWIGO WA CEKENA KIDATO CHA NNE – 2015

**Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari**

**MAAGIZO:**
1. Jibu maswali **manne** pekee.
2. Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
3. Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizosalia yaani Hadithi Fupi, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu **moja**.
5. Kila swali lina alama **20**.
6. Mtihini huu alama **80**.



**SEHEMU YA A**: **Kidaaga Kimemwozea: Ken Walibora**

1. "……. Kidagaa kimetuozea kwa kutamaushwa na usaliti wa viongozi wa baada ya uhuru."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Taja na ufafanue sifa **nne** za viongozi wanaorejelewa. (alama 8
(c) Kwa kurejelea riwaya hii, eleza ni kwa njia gani viongozi wamedhirishwa kama wasaliti. (alama 8)

**SEHEMU YA B: Damu Nyeusi na Hadithi Nzingine**

2. "Nashangaa vile kwetu tunavyoabudu watu hao wasiojali."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua hulka za msemewa. (alama 4
(c) Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)

3. Diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine imesheheni uozo wa kijamii unaolemea nchi zinazoendelea. Jadili. (alama 20)

**SEHEMU YA C: Mastahiki Meya: Timothy Arege**

4. "…….. Dawa ya adui nikummegea unachokula."
(a) Eleza muktdha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Ni maudhui yepi yanayojitokeza katika dondoo hili? Jadili. (alama 4)
(c) Fafanua mifano mingine **mitano** ya maudhui hayo uliyoyatoa katika (b). (alama 4)
(d) Eleza sifa **nne** za msikilizaji wa kauli hii. (alama 4)

5. Tamthilia ya Mstahiki Meya ni kioo cha changamoto nyingi za Kiafrika. Jadili. (alama 20)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

6.
1. Ole wangu! Ole wangu, nisikize Mola wangu,
Lipokee ombi langu, wanisikize wenzangu,
Washike ujumbe wangu, uloleta Mola kwangu,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

2. Amri kumi za Mola, mumekwisha zikiuka
Ndipo hamuwezi lala, mumekwisha vurugika,
Mumemsahau Mola, ndipo nanyi mwasumbuka,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

3. Mwaabudu mashetani, ushirikina ni mwingi,
Munaiba hadharani, waongo nao ni wengi,
Mwajawa na taraghani, na wazimu mwingi mwingi,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

4. Mwauana ovyoovyo, mwasemana ndivyo sivyo,
Fitina nazo zilivyo, mwarogana vivyo hivyo,
Matusi ni vile sivyo, munaisha ka isivyo,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

5. Kuna dawa za kulevya, na hata pombe haramu,
Na ukimwi nakujuvya, unaua wanadamu,
Na mimba nazo kuavya, watoto ni marehemu,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

6. Wengine nao hudai, waoe jinisi moja,
Ati mwingine hafai, heri sawia ya mja,
Haya maoni ni hoi, tupinge kila mmoja,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.



7. Ploti mwazinyakua, na viwanja vya mipira,
Makaburi mwala pia, mabibi mwateka nyara,

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Ibada zikifikia, mwafurika kwa majira,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

8. Wengi tuwachaguao, si vongozi ni waizi,
Tamaa walio nao, yaongoza maamuzi,
Mishahara ile yao, huongezwa kila mwezi,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

9. Usalama hatunao, wasiwasi umezidi,
Waja kiwa makazio, huogopa magaidi,
Mabomu walipuao, huruma wamekaidi,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

10. Beti kumi namaliza, dua yangu imetimu,
Mungu amekwisha anza, kuhukumu mwanadamu,
Wote walojipotoza, waiepuke hukumu,
Nyakati tunazoishi, ni Sodoma na Gomora.

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Maswali

1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)
2. Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari kadha. Taja na ueleze bahari zozote **tatu**. (alama 3)
3. Taja na ueleze mbinu **tatu** za lugha zilizotumiwa katika ubeti wa **kwanza**. (alama 3)
4. Eleza sababu ya mshairi kutumia alama
   (a) Ya ritifaa katika ubeti wa **nne**. (alama 2)
   (b) Tumbua uhuru wa kishairi uliotumika katika ubeti wa **tisa** mshororo wa tatu na ueleze umuhimu wake. (alama 2)
5. Andika ubeti wa **sita** kwa lugha tutumbi. (alama 4)
6. Taja mifano **mitatu** ya uozo anaolalamikia mwandishi. (alama 3)
7. Eleza toni ya mwandishi. (alama 2)

**SEHEMU YA E: USHAIRI**

**SIWE?**

7.

1. Siwe ulosema jana, ya kuwa u mashuhuri?
Ya kuwa wajuwa sana, aidha huna kiburi?
Nchini wajulikana, mwanasiasa mahiri,
Bungeni tukuajiri?

2. Siwe ulotushawishi, kwa chumvi na kwa sukari,
Na matamu matamshi, ukaziteka suduri,
Ukanena penya moshi, moto ndiyo yakwe siri,
Nawe ndiye hiyo nari?

3. Siwe uloji'ta moto, uwakao biribiri,
Kamba 'tatia fukuto, Litakalo leta kheri',
Utatufunua mato, Maisha yawe mazuri,
Tukupe kura waziri?

4. Siwe ulosema hayo, na mengi ukabashiri,
Ukamba wafata nyayo, nyayo ziso utiriri,
Tusiwe na wayowayo, wa kufikirifikiri,
Tukuachie ujari?



5. Siwe tulokuinua, Mabegani kama mwari,
Tungawa twalemelewa, waume tukajasiri,

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Kamba tukikuchaguwa, mema kwetu yatajiri,
Tukakeyi kusubiri?

6. Siwe ulotugeuka, kwamba leo uwaziri,
Wajiona melimuka, tena ukawa ayari,
Walaghai ukicheka, ukuu umekughuri,
Leo mekuwa hodari?

7. Siwe ulojawa raha, za hino yetu sayari,
Ukawa ja vile shaha, hatukupati shauri,
kutuona ni karaha, wakatiwo twahasiri,
Ushakiya msitari?

8. Siwe uliyetughura, ukafunga na safari,
Ukaelekea bara, Kwa wenzio matajiri,
Ukatuacha majura, na tama kukithiri,
Kanama Ushaghairi?

9. Siwe uliyetuasi, ukenda pasi kwaheri,
Mbona hutwambii nasi, tukajua yetu shari,
Leo una masidisi, husemi na aso gari,
Ndio mezidi jeuri?

10. Siwe'lotwaa mgwisho, ukawa wajifakhiri?
Chenye mwanzo kina mwisho, hilo wajuwa dhahiri,
Vyaja kutoka vitisho, kwani hayo sidahari,
Mambo mengimdawari?

11. Siwe utakayeiza, mwishowo ukidhihiri,
Siku itayoteleza, kuja kwetu ansari,
Kuja kutubembeleza, kwa nyunga nalo khamri,
Tauya nazo nadhiri.

Maswali

(a) Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? (alama 2)

(b) Taja na ueleze bahari tatu za shairi hili? (alama 3)

(c) Onyesha jinsi mtunzi alivyotumia idhini ya kishairi. (alama 3)

(d) Taja na ufafanue tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi hili. (alama 2)

(e) Anayerejelewa alibadilika vipi? Eleza. (alama 4)

(f) Andika ubeti wa tisa kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(g) Mshairi ana maana gani kwa kusema.
  (i) Wakatiwo twahasiri. (alama 1)
  (ii) Ukaziteka suduri. (alama 1)

**SEHEMU YA E: Fasihi Simulizi**

8. (a) Eleza maana ya miviga. (alama 2)

(b) Eleza sifa **tano** za miviga. (alama 5)

(c) Miviga ina udhaifu gani. (alama 3)

(d) Fafanua umuhimu wa ngomezi katika jamii. (alama 10)

(e) Eleza vizingiti **viwili** vinavyokumba ngomezi. (alama 4)